



## **TANGAZO KWA UMMA**

### **BENKI KUU YA TANZANIA YACHUKUA USIMAMIZI WA BENKI YA TWIGA**

Kwa mamlaka iliyopewa chini ya kifungu cha sheria namba 56(1)(g)(i) na 56(2) (a)-(d) cha Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, Benki Kuu ya Tanzania imeamua kuchukua usimamizi wa benki ya Twiga (Twiga Bancorp Limited) kuanzia tarehe 28 Oktoba 2016.

Uamuzi huu umechukuliwa baada ya kubaini kuwa benki ya Twiga ina upungufu mkubwa wa mtaji kinyume na matakwa ya sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 na kanuni zake. Upungufu huu wa mtaji unahatarisha usalama wa sekta ya fedha na pia kuendelea kutoa huduma za kibenki kwa benki ya Twiga kutahatarisha usalama wa amana za wateja wake.

Kutokana na uamuzi huo, Benki Kuu ya Tanzania imeisimamisha Bodi ya Wakurugenzi na uongozi wa benki ya Twiga na imemteua Meneja Msimamizi ambaye atakuwa na jukumu la kusimamia shughuli za benki ya Twiga kwa kipindi ambacho itakuwa chini ya usimamizi wa Benki Kuu. Pia, umma unaarifiwa kuwa katika kipindi kinachokadiriwa kufikia wiki moja kuanzia siku ya taarifa hii, shughuli za utoaji wa huduma za kibenki za benki ya Twiga zitasimama ili kutoa nafasi kwa ajili ya kupanga taratibu za uendeshaji wa benki hiyo.

Benki Kuu ya Tanzania inapenda kuuhakikishia umma kuwa itaendelea kulinda maslahi ya wenye amana katika mabenki kwa lengo la kuleta ustahimilivu katika sekta ya fedha.

**BENKI KUU YA TANZANIA**

**28 Oktoba, 2016**

